



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA



**TANGAZO LA ZABUNI/MAFUNDI UJENZI
(MARUDIO)**

1. TAREHE: 30.08.2023
2. JINA LA MRADI: **UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BULAMBA**
3. CHANZO CHA FEDHA: **SERIKALI KUU**
4. KAZI INAYOHITAJIKA:
Ujenzi wa majengo yafuatayo katika ujenzi washule ya wasichana Bulamba kwa kufuata ramani iliyotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo inapatikana katika ofisi ya Mkurugenzi Halmashauri ya wilaya ya Bunda.

S/no	AINA YA MAJENGU	IDADI YA MAJENGU
1	Jengo la maabara ya Fizikia na jiografia	1
2	Jengo la utawala	1
3	Jengo la vyoo vya wanafunzi	1
4	Chumba cha Jenereta	1
5	Bwalo/Ukumbi	1
6	Nyumba za waalimu (2in 1)	1
7	Mabweni @ wanafunzi 120	8
8	Chumba cha wagonjwa sick bay)	1

5. UTAALAMU UNAOHITAJIKA:
 - I. Angalau Uzoefu wa miaka mitatu (3) katika kazi za ujenzi wa majengo ya serikali
 - II. Uwezo wa kusoma ramani
 - III. Fundi mwenye elimu ya Ufundu FTC au Uhandisi ni lazima kwa Jengo la Utawala na Bwalo
 - IV. Fundi mwenye elimu ya Ufundu FTC au Uhandisi atazingatiwa na atapewa kipaumbele kwenye ujenzi wa mabweni, maabara, madarasa na Vyoo
 - V. Fundi ni lazima awe na vifaa kama Concrete mixer na poker vibrator na Grinder ya kukatia Nondo na mashine ya welding.
 - VI. Awe raia wa Tanzania.
 - VII. Jengo la utawala na Bwalo fundi anatakiwa kuwa na mtaji usiopungua Milioni 10.

- VIII. Mafundi wote wanatakiwa kuwa na uwezo wa kugharamia vibarua mpaka hatua ya msingi, kwani malipo ya kwanza yatafanyika baada msingi kukamilika.
- IX. Fundi anatakiwa kuwa na Nguvu kazi ya kutosha.

6. MALIPO:

Malipo kwa awamu yatafanyika baada ya kukamilika na kukaguliwa kwa kazi kwa kila awamu na kuthibitishwa na msimamizi/mhandisi wa Halmashauri

7. MCHAKATO WA ZABUNI:

Fundi/mtoa huduma kwa kazi hii atachaguliwa kupitia zabuni ya wazi ya ushindani. Zabuni zitafunguliwa katika mkutano wa ufunguzi wa zabuni na kufanyiwa tathimini kwa kutumia vigezo vifuatavyo:

- i. Uzoefu wa miaka mitatu
- ii. Ushahidi wa ubora wa kazi za zamani alizowahi kufanya
- iii. Gharama iliyopendekezwa
- iv. Masharti yote yaliyotajwa hapo juu.

8. MAHALI PA KUPATA NYARAKA ZA ZABUNI:

Nyaraka za zabuni zitapatikana katika ofisi ya Katibu wa bodi ya zabuni siku za kazi kuanzia saa mbili na nusu (2.30)asubuhi hadi saa tisa na nusu (9.30) alasiri

9. TAREHE YA MWISHO YA KUWASILISHA NYARAKA:

Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha nyarakani 13/09/2023 saa nne kamili (4.00) asubuhi. Hakuna zabuni itakayopokewa baada ya tarehe na muda huu.

10. MAHALI PA KUPELEKA ZABUNI:

Bahashaifungwe vizuri na kuwasilishwa kwa mkono au itumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU BODI YA ZABUNI
 HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA
 S.L.P 126 BUNDA - MARA**



Oscar Kapinga

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

BUNDA

**(G.M. MKURUGENZI MTENDAJI (W)
 BUNDA)**